

# **Je Mungu Anatutaka (Wakristo) Kutoa Fungu La Kumi?**

**(Does God Expect Us Christians  
To Tithe?)**

**Na**

**Alex S. Silvester**

# **Je Mugu Anatutaka (Wakristo) Kutoaa Fungu La Kumi?**

**Na**

**Alex S. Silvester**

**Juni 19, 2018**

# Je Mungu Anatutaka (Wakristo) Kutoa Fungu La Kumi?

Je unafahamu kwamba katika Agano Jipya hakuna agizo, sheria, amri, wajibu wa moja kwa moja wa kutoa fungu la kumi? Ni kweli! Hatupo chini ya agizo kama hilo. Lakini wapo watu wanaowashinikiza waumini wao kutoa fungu la kumi hasa ndugu zetu wa vikombe vingi, hii inaonyesha ni jinsi gani watu wamesoma maandiko vibaya. Fungu la kumi ilikuwa ni sehemu ya Agano la Kale na sasa haina nguvu chini ya Agano Jipya. Yesu alitimiza sheria ya zamani kwa kuiondoa na kuibadilisha katika sheria mpya. *“Akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepo tena, akaigongomea msalabani; akiisha kuzivua enzi na mamlaka na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaaba huo.”* (Kol. 2:14-15). Fungu la kumi lilikuwa ni sehemu ya Sheria ya Kale ambayo iliondolewa. Sasa unapata kwamba madhehebu bado wanalazimisha watu kwamba ni lazima kutoa fungu la kumi.

Katika Agano Jipya tunapaswa ku:

- Kutoka kulingana na tulivyofanikiwa. *“Siku ya kwanza ya juma kila mtu kenu na aweke akiba kwake kwa kadiri ya kufanikiwa kwake, ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja.”* (1 Cor. 16:2). Hatuwezi kupata fungu la kumi katika Agano Jipya.
- Tutoe kama tulivyokusudia moyoni mwetu. *“Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo mkunjufu.”* (2 Kor. 9:7). *“Mungu humpenda atoaye kwa moyo wa ukarim”* Na sio mtoa fungu la kumi mkarimu. (2 Kor. 9:7).
- Au tunapaswa kutoka eti kwa sababu imetulazimu. (2 Kor9:7).

Mungu ametuacha sisi kuamua changizo yake itakuwaje na hajatao agizo lolote kuhusiana na asilimia. Ni wito wetu. Tunapaswa kutoa kiwango tunachochagua na ambacho kinafaa.

*“Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo mkunjufu.”* (2 Kor. 9:7).

Yesu alisema hili kuhusiana na utoaji wetu:

*“Wapeni watu vitu nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwasukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho*

*mtakachopimiwa.*” (Luka 6:38). Kanuni kama hii ilikuwa na ukweli chini ya Agani la Kale Mungu alipowaambia Waisraeli:

*“Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema BWANA wa majeshi mjue kama sitawafunguliaa madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka hata isiwepo nafasi ya kutosha au la.”* (Mal.3:10).

Tena mfumo wa utoaji zaka sio lazima chini ya Agano Jipya, hataivyo mfumo unabaki kuwa kama ule wa kwanza; kadiri tumtoleavyo Mungu, ndivyo anavyotupa zaidi; *“kipimo cha kujaa na kushindiliwa na kusukwasukwa hata kumwagika.”* Marafiki zetu na makanisa yalioko jirani ni lazima warudi kwenye Biblia na kujifunza kwa kuchimba kile ambacho Mungu anawaagiza watu wake kuhusiana na kutoa. Sio kuwalazimisha waumini kutoa fungu la kumi. Hata ivyo sisi sio wafuasi wa Musa bali wa Kristo.







